



Akademia ya Afrika ya Lugha (ACALAN) Hamdallaye ACI 2000 Porte 223 Rue 394, Bamako-Mali, Barua pepe: [acalan@africa-union.org](mailto:acalan@africa-union.org) Tovuti: [www.acalan-au.org](http://www.acalan-au.org) Simu. +223 20 29 04 59 Tarakilishi +223 20 29 04 57

## Taarifa kuhusu Warsha ya Kuwianisha Mifumo ya Uandishi ya lugha maarufu tambuka-mpaka za Kiewe, Kisoninke na Kisonghay

### Utangulizi

Akademia ya Afrika ya Lugha (ACALAN), kwa kushirikiana na Kituo cha Taaluma za Historia kwa Masimulizi (CELHTO), na Mfuko wa KARANTA, iliandaa warsha ya uwianishaji wa mifumo ya uandishi ya lugha maarugu tambuka-mpaka za Kiewe, Kisoninke na Kisonghay, huko Ouagadougou, Burkina Faso, kuanzia tarehe 11 hadi 13 Maachi 2020.



Malengo ya Warsha yalikuwa:

- i. Kusawazisha tofauti zilizopo za kiuandishaji;
- ii. Kuunda alfabeti moja na mfumo mmoja wa kuandika lugha hizo;
- iii. Kuandaa mfumo sanifu wa kuandika kila lugha;
- iv. Kuunda leksikoni ndogo ya kila lugha;
- v. Kusawazisha kanuni za kisarufi;
- vi. Kuweka mikakati na taratibu za kukamilisha na kusambaza kanuni zilizowianishwa.

Warsha hiyo ilihudhuriwa na washiriki kutoka lugha tatu husika, Raisi wa Baraza la ACALAN la Wanataaluma, watumishi wa Sekretarieti ya ACALAN, pamoja na Katibu Mkuu mwenye dhamana na Maendeleo ya Lugha za Taifa na Elimu ya Uraia aliyewakilisha Wizara ya Elimu ya Taifa, Elimu ya Watu Wazima na Maendeleo ya Lugha za Taifa ya Jamhuri Iya Burkina Faso (MENAPLN).

Katibu Mtendaji wa Akademia ya Afrika ya Lugha, Dkt Lang Fafa Dampha aliwakumbusha wajumbe wa Kamisheni za Lugha Maarufu Tambuka-mpaka kuhusu umuhimu wa kufanya kazi kwa ushirikiano na Vyombo vya Lugha vya Kitaifa . Alitoa ushauri kwa nchi zinazotumia lugha moja kushirikiana ili kuziendeleza lugha zao kwa kuwianisha mifumo ya uandishi ya lugha hizo. Alieleza kwamba Vyombo vya Kitaifa vya Lugha vinavyofanya kazi kama dawati la ACALAN vina jukumu la kuwakilisha taasisi hiyo kwenye nchi husika katika masuala yote ya lugha vikishirikiana na Kamisheni za Lugha Tambuka-mpaka. Aliwakaribisha na kuwaomba wajumbe waendeleo kuwa mabalozi wa ACALAN, watoe habari kwa usahihi na wahakikishe kwamba malengo ya ACALAN yanatekelezwa kwa ufanisi.

Rais wa Baraza la Wanataaluma wa ACALAN, Profesa Sammy Beban Chumbow, alieleza kuhusu umuhimu wa kuwianisha mifumo ya uandishi ya Lugha za Kiafrika pamoja na jukumu la Kamisheni za Lugha Maarufu Tambuka-mpaka. Alitoa ufafanuzi kuhusu dhana ya *tambuka-mpaka* na ya *lugha maarufu* kwa kutofautisha dhana hizo mbili. Aidha alieleza kuhusu sifa za lugha maarufu tambuka-mpaka, vigezo vya kuzitambua, na majukumu na kazi za Kamisheni za lugha hizo. Profesa Chumbow pia alizungumza kuhusu hadhi ya lugha “kubwa” kama vile Kizulu cha Afrika ya Kusini, Kisango cha Jamhuri ya Afrika ya Kati, na Kiibo cha Nigeria na jukumu la ACALAN kwa lugha hizo.

Wajumbe wa Kamisheni za Lugha Maarufu Tamuka-mpaka tatu waliwasiisha taarifa za nchi zao kuhusu uwianishaji wa mifumo ya uandishi ya lugha hizo ambazo ni Kiewe, Kisonghay na Kisoninke, katika kila nchi. Uwasilishaji ulifanyika kwa kuzingatia maeneo matatu : kilichafanyika; hali ilivyo sasa ; na kinachopaswa kufanyika (mikabala).

Kutokana na uwasilishaji huo, ilibainika kuwa lugha maarufu tambuka-mpaka za Kiewe, Kisoninke na Kisonghay zina mifumo tofauti tofauti ya uandishi kulingana na ukanda ambako lugha hiyo huzungumzwa ndani ya nchi moja, na kwamba kwa baadhi ya nchi mifumo hiyo ya kiuandishi imewekwa kisheria.

Katika siku ya pili ya Warsha, tarehe 12 Machi, washiriki walijigawa kulingana na Kamisheni za lugha zao na kufanya kazi ya uwianishaji wa mifumo ya uandishiji ya lugha husika.

Yafuatayo ni matokeo ya Warsh hiyo:

- i. Tofauti za kiuandishi , zilisawazishwa;
- ii. Alfabeti moja na mfumo mmoja wa uandishi kwa lugha hizo, uliundwa;
- iii. Mfumo sanifu wa uandishi kwa kila lugha , uliandaliwa;
- iv. Leksikoni ndogo ya kila lugha , iliundwa;
- v. Kanuni zilizosawazishwa za kisarufi , ziliundwa;
- vi. Mikakati na taratibu za kukamilisha na kusambaza kanuni zilizowianishwa, ilijadiliwa

**Akademia ya Afrika ya Lugha (ACALAN),  
Bamako - Mali, 14 March 2020**